# Elimu Mjumuisho

Kijitabu cha Utangulizi



## Muongozo kwa wakufunzi wa walimu

Imeandaliwa na:
**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar**
Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu Norway
Jumuiya ya Makuzi ya Awali ya Mtoto Zanzibar

Imeandaliwa na:
Mtandao wezeshi wa Elimu, Mei 2016, ulifanyiwa marekebisho Septemba 2022

**Elimu Mjumuisho: Kijitabu cha Utangulizi**
Nyenzo ya mafunzo ya ualimu kwa wakufunzi wa walimu
Toleo la 1

Nyenzo hii ya mafunzo ya ualimu mwanzoni iliandaliwa kwa ushirikiano baina ya Jumuiya ya Watu weney Ulemavu ya Norway (NAD), Jumuiya kwa Ajili ya Watu wenye Ulemavu wa Akili ya Norway (NFU) na Mtandao wezeshi wa Elimu (EENET), Wizara ya Elimu Zambia na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar.

Toleo hili la Zanzibar limeandaliwa kwa ajili ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (WEMA) kwa msaada wa Taasisi zifuatazo:

Kazi hii imeidhinishwa kwa Leseni ya Kimataifa ya *'Creative Commons Attribution-NonCommercial-ShareAlike'* 4.0. Ili kuona nakala ya leseni hii, tembelea mtandao wa:
http://creativecommons.org/licenses/by-nc-sa/4.0/

# Yaliyomo

Shukrani na vyanzo vya taarifa.......... iv

Taarifa Muhimu .......... v

Vifupisho.......... vi

Dibaji.......... vii

A. Muongozo wa mafunzo .......... ix

B. Warsha za Mafunzo ya Wakufunzi (ToT) .......... xvi

C. Mbinu .......... xvii

D. Ujuzi wa mawasiliano .......... xix

E. Nini Elimu Mjumuisho? .......... xx

F. Mfumo wa Kujitathmini kwa walimu na skuli katika mafunzo ya elimu mjumuisho(IETT).......... xxi

G. The Muktadha wa Kizanzibari.......... xxii

H. Walengwa wa mafunzo haya .......... xxiv

# Shukrani na vyanzo vya taarifa

Nyenzo katika utangulizi huu na seti zinazoambatana za moduli za mafunzo zinatokana na nyenzo zilizoandaliwa na kufanyiwa majaribio na timu ya EENET kwa mashirikiano na wadau wengine katika maeneo mbalimbali barani Afrika, Asia na Ulaya. Hizi ni pamoja na:

- Warsha ya mafunzo ya wakufunzi iliyoandaliwa kwa ajili ya Diakonia, Palestine, Julai 2011;
- ‘Elimu Mjumuisho: Muongozo kwa wakufunzi wa walimu’, ulioandaliwa kwa ajili ya Shirikisho la Kimataifa la Ulemavu (HIF), Kambodia, 2011;
- Mpango wa mafunzo kwa wakufunzi ulioandaliwa kwa ajili ya Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Kuhudumia Watoto (UNICEF), Macedonia, 2012–13;
- Programu ya mafunzo kwa wakufunzi iliyoandaliwa kwa ajili ya UNICEF, Libya, 2012–2013;
- ‘Utangulizi wa Elimu Mjumuisho: Muongozo kwa wakufunzi wa walimu’, ulioandaliwa kwa ajili ya HIF, Liberia, 2012–13;
- ‘Misingi ya Ufundishaji: Mafunzo kwa waelimishaji katika umahiri wa kufundisha’, iliyoandaliwa kwa ajili ya Save the Children, 2017;
- ‘Elimu Mjumuisho: Mafunzo ya awali kwa walimu’, yaliyoandaliwa na kufanyiwa majaribio kwa Leonard Cheshire, Tanzania na Uganda, 2017–2018;
- 'Elimu Mjumuisho Mafunzo ya walimu kazini: Muongozo wa wakufunzi wa walimu' ulioandaliwa na kujaribiwa kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (MoEVT), Zanzibar, Wizara ya Elimu Zambia, Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu Norway (NAD) na Jumuiya kwa Ajili ya Watu wenye Ulemavu (NFU), 2016-2019.

Jumuiya kadhaa, ikiwa ni pamoja na EENET, MoEVT, NAD na NFU, pamoja na idadi kubwa ya watu binafsi, wanashirikishwa katika mchakato wa kuandaa na kupima moduli za mafunzo. Hatuwezi kuorodhesha kila mtu hapa, lakini tunatoa shukrani za dhati kwa juhudi na dhamira zao za kusaidia maendeleo ya elimu mjumuisho Zanzibar.

# Taarifa Muhimu

Nyenzo kama vile vijitabu, fomu, kadi za shughuli na karatasi zilizotajwa katika vipindi vya mafunzo zinaweza kupatikana mwisho wa kila moduli.

Katika moduli zote, picha na michoro zimefafanuliwa ili kuwasaidia wasomaji wenye ulemavu wa uoni.

Neno 'mwanafunzi' linatumika katika moduli zote za mafunzo kumaanisha watoto, wanafunzi na vijana. Vilevile, neno 'skuli' mara nyingi hutumika kwa ufupi na linaweza kutafsiriwa kujumuisha mazingira ya kielimu katika ngazi zote: mazingira ya makuzi ya awali ya mtoto (ECD), skuli ya maandalizi, msingi, sekondari, vyuo , taasisi za elimu ya juu, na mazingira mengine yanayotoa elimu.

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| JWWU | Jumuiya za Watu Wenye Ulemavu |
| MAM | early childhood development Makuzi ya Awali ya mtoto |
| EENET | Mtandao wezeshi wa Elimu |
| HIF | Shirikisho la Kimataifa la Ulemavu |
| MEM | Mratibu wa Elimu Mjumuisho |
| MBK | Mpango Binafsi wa Kielimu |
| INSET | Mafunzo Kazini |
| WEMA | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali |
| NAD | Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu Norway |
| NFU | Jumuiya kwa Ajili ya Watu wenye Ulemavu wa Akili ya Norway |
| NORAD | Shirika la Maendeleo la Norway |
| MM | Mkufunzi Mkuu |
| SSI | Sight Savers International |
| SUZA | Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar |
| TMU | Taasisi ya Mafunzo ya Ualimu |
| ToT | Mafunzo ya wakufunzi |
| UNESCO | Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni |
| UNICEF | Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Kuhudumia Watoto |
| USAID | Msaada wa Marekani |
| WHY | Nyumba ya Ulimwengu kwa Vijana |
| ZAPDD | Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu wa Akili Zanzibar |

# Dibaji

Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu Norway (NAD) na washirika wake wa Zanzibar wanafanyakazi na Mtandao Wezeshi wa Elimu (EENET) kuandaa na kufanyia majaribio mbinu ya mafunzo ya ualimu kuhusu elimu mjumuisho ili itumike katika mazingira ya watu wenye kipato cha chini na kati. Matokeo yake yatoe kozi yenye ubora wa juu wa mafunzo ya ualimu katika elimu mjumuisho.

Kifurushi hiki cha mafunzo kimeandaliwa ili kuwaendeleza wakufunzi ambao tayari wamo ndani ya mfumo wa elimu kama walimu, wakufunzi wa walimu na viongozi kwa ajili ya ujumuishaji.

Moduli zinazotumika zinapaswa kuwiana kwa karibu na mageuzi ya mtaala wa mafunzo ya ualimu, na kuchangia moja kwa moja mabadiliko ya kimfumo yanayohitajika ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wanaweza kupata elimu kushiriki na kuendelea katika elimu. Gharama za programu hii zinaweza kufanywa kuwa ndogo kwa kuchagua wakufunzi wakuu ambao tayari wameshaajiriwa katika kazi zinazosaidia, kutoa mafunzo na/au kusimamia walimu.

Mbinu ya mafunzo inayotumika katika kufundishia moduli hizi isiwe ile ya kutumia walimu waliofunzwa ili nao wakawafunze wenzao ambayo mara nyingi haitoi fursa kwa walimu kujifunza kwa hali ya ubora unaohakikisha mabadiliko ya kweli na endelevu katika mitazamo na utendaji wao skuli[2]. Mbinu za kutumia walimu waliofunzwa ili kuwafunza wengine, mara nyingi zinakuwa ni za muda mfupi na za haraka haraka. Mara nyingi mbinu hizi zinajumuisha kozi fupi za mara moja tu, na zinaweza kuwafikia washiriki wengi, ambao wataweza kujifunza kwa ufupi na kwa nadharia tu lakini  mafunzo yanakuwa ya kijuu juu tu na kutoa nafasi ndogo kwa washiriki kufanya uchunguzi, kujadili au kuangalia matendo ya ujumuishaji katika uhalisia wake. Nyenzo mara nyingi hutengenezwa na wataalamu wa nje na huwa ‘hazimilikiwi’na wakufunzi wenyewe.’ Ingawa mafunzo hayo yanaongeza ufahamu wa walimu, lakini huwa yana upungufu katika utendaji wao wa kazi.

## Muhtasari wa sifa kuu za mbinu za mafunzo

Mbinu hii imebuniwa ili:

- Kujenga kada ya wakufunzi wakuu wenye uzoefu, ujuzi na kujiamini ambao wana uwezo wa kutoa mafunzo kwa walimu na walimu wanafunzi na kuyafanya mafunzo yanayoendelea kuwa bora zaidi. Mafunzo haya huwa yanaendelea angalau kwa miaka miwili.
- Kutengeneza nyenzo za mafunzo zinazoendana na muktadha ambao huandaliwa kwa ushirikiano na hivyo humilikiwa na wadau wakuu wa elimu, wakiwemo wakufunzi.
- Kukuza matumizi ya mbinu ya mafunzo ya ualimu ambayo inatoa kipaumbele zaidi vitendo kuliko nadharia, inakuza ujifunzaji kwa vitendo, na kujenga uwezo wa walimu kuwa wabunifu na watatuzi wa matatizo wanaotafakari kwa kina.
- Kutumia mbinu jumuishi katika kujifunza, kwa kuanza na misingi ya awali ya elimu mjumuisho na kuendelea na mada ngumu zaidi na mahususi. Hii huwasaidia walimu hatua kwa hatua kujenga kujiamini katika kujifunza.
- Kuhakikisha kwamba mafunzo ya ualimu kazini yanahusiana kwa karibu na/au yanaathiri mabadiliko endelevu katika mafunzo ya kabla ya ajira, kwa kuorodhesha wakufunzi ambao wameajiriwa na taasisi za mafunzo ya ualimu na kwa kudumisha uhusiano na taasisi hizo kubadilishana nyenzo na taarifa.

## Muda

Kimsingi, panga utaratibu wa kusambaza mafunzo ya moduli zote kwa kufuatana kwa muda wa miaka miwili. Hii inahitaji wakufunzi wakuu kujifunza na kusaidia kurekebisha moduli za mafunzo, kuhudhuria warsha mbili au tatu za wakufunzi kila mwaka, na kupanga vipindi vya mafunzo ya walimu wote katika skuli baada ya kila warsha ya mafunzo ya wakufunzi.

Ikiwa hii haiendani na muktadha wako, ainisha a) muda zaidi, au b) maelewano kuhusu idadi ya moduli zitakafundishwa kwa muda huo.

# A. Muongozo wa mafunzo

Muongozo huu wa mafunzo una kijitabu hiki cha utangulizi pamoja na moduli 7 na moduli ya nyongeza juu ya ‘Ujumuishaji wa Wanafunzi wenye Mahitaji ya Ziada’. Moduli nyengine tano fupi pia zimeandaliwa kwa ajili ya kukuza ustawi wa kihisia wa wanafunzi wanaopitia changamoto za kutokuwa na makaazi na upotevu, kupunguza hatari ya maafa, ufuatiliaji na tathmini, kujifunza nyumbani na nidhamu endelevu.

Wakufunzi wakuu hupewa yafuatayo katika kila moduli:

- maudhui na mbinu wanazohitaji kujifunza na kufanya mazoezi wakati wa warsha za wakufunzi na kisha kuzitumia wakati wa warsha za walimu na walimu wanafunzi;
- muongozo wa kutoa mafunzo kwa mujibu wa maelekezo na kufanya maerekebisho ya warsha katika kazi zao za mafunzo na walimu na walimu wanafunzi;
- mawazo ya namna ya kuendelea kufanyia kazi baadhi ya mada zilizoibuliwa katika warsha, na jinsi ya kupanua shughuli nyengine baada ya warsha.

Moduli hizo zinasaidia mbinu ya mafunzo ambayo huwasaidia walimu kuwa wabunifu na wenye kujiamini katika kutatua matatizo kupitia:

- **Kujifunza kwa vitendo.** Moduli zote zina shughuli shirikishi, zinazomlenga mwanafunzi/mshiriki ambazo zinahitaji washiriki kutafakari juu ya maisha na uzoefu wao wenyewe na kutatua matatizo kwa jozi na katika vikundi. Washiriki kamwe hawaambiwi tu majibu ya maswali. Kama ilivyo wanafunzi walio mahiri katika skuli, ni lazima watoe majibu wenyewe, kwa msaada wa mkufunzi.
- **Kazi za utafiti tatuzi**. Katika kila moduli kuna kazi ya utafiti tatuzi. Katika skuli yao ya majaribio, wakufunzi wakuu hufanya uchunguzi mdogo kuhusu tatizo ambalo wamelianisha na/au kulijaribu kwa njia mpya. Wanafanya kazi na kamati ya Elimu Mjumuisho ya Skuli (SIT), mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli (IECo) na wanajamii kuweka kumbukumbu na kushiriki uchunguzi au kupeana taarifa za uchunguzi na wenzao kwenye warsha inayofuata ya mafunzo.
- **Ujifunzaji Jumuishi.** Moduli hizi zinatumia mbinu jumuishi katika kujifunza. Zinaanza na misingi ya elimu mjumuisho na kuendelea kwenye mada ngumu zaidi na mahususi. Hii huwasaidia washiriki kujenga kujiamini hatua

kwa hatua katika kujifunza  na kutekeleza matendo ya ujumuishaji na kutatua changamoto za ujumuishaji bila ya kuweka matarajio makubwa na ya kutatanisha kwao baada ya warsha moja tu.

- **Kujifunza kushirikiana.** Mafunzo hayatarajii washiriki kujifunza kila kitu na kutatua kila tatizo wenyewe. Kwa mfano, kuna moduli zinazosaidia washiriki kufanya kazi kwa mashirikiano ili kuunda Kamati za Elimu Mjumuisho za Skuli (SITs) na Waratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli (IECos). Kwa kuongezea, moduli zote zinahimiza utafiti tatuzi ambao washiriki wanafanya kazi na wenzao, wazazi, wanafunzi na jamii kuchunguza na kushughulikia changamoto za ujumuishaji.

Wakufunzi wanashauriwa kufuata hatua zilizowekwa katika muongozo ili kuhakikisha kuwa kuna uelewa wa kina juu ya ujumuishaji. Muongozo wa mafunzo umetayarishwa na kujaribiwa katika programu ya mafunzo ya wakufunzi ya elimu mjumuisho na wakufunzi wakuu. Wakufunzi wakuu hutumia muongozo huo kuwaongoza walimu wao wa mafunzo kazini katika skuli, na walimu wanafunzi katika taasisi za mafunzo ya ualimu (TTIs). Moduli ya nyongeza ina taarifa juu ya kusaidia wanafunzi wenye mahitaji ya ziada na ushauri kuhusu ulemavu maalum.

Jaduweli lifuatalo linatoa maelezo mafupi ya moduli zote katika mtiririko wa mafunzo ya elimu mjumuisho. Pia inaelezea maeneo ya mada ambayo yanafundishwa katika kila moduli. Tafadhali kumbuka kuwa kufanya utafiti tatuzi juu ya mada zinazofundishwa ni sehemu ya moduli zote.

| Moduli | Maelezo mafupi | Mada kuu zilizomo |
|---|---|---|
| **Moduli ya 1:**<br>**Utangulizi wa Elimu Mjumuisho** | Hutambulisha dhana na nadharia za elimu mjumuisho na msingi wa kinadharia wa utekelezaji wake; na inatambulisha mbinu shirikishi za kujifunza ambazo washiriki watapata uzoefu katika kipindi chote cha mafunzo. | Ufafanuzi na majadiliano ya elimu mjumuisho<br>Miongozo ya sera na sheria<br>Mitindo ya kujifunza<br>Kujifunza kwa umakini<br>Vikwazo vya elimu mjumuisho vikiwemo ubaguzi, mitazamo ya walimu na vikwazo vya kimfumo.<br>Utafiti tatuzi na uchunguzi wa kuthamini. |
| **Moduli ya 2:**<br>**Kamati za Elimu Mjumuisho za Skuli na Wajibu wa Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli.** | Hutoa taarifa kwa walimu na wadau wengine muhimu, kama vile wafanyakazi wa skuli, Maafisa Elimu wa Wilaya na Mkoa, wanajamii na wadau wengine wanaotaka kupanga, kuendeleza na kusimamia SIT katika Skuli zao.<br>Moduli hii pia inaangalia jukumu la Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa skuli, jinsi anavyoweza kuratibu mahitaji ya ziada na shughuli za elimu mjumuisho, na jinsi anavyoweza kuwa chachu ya mabadiliko kuelekea mfumo wa elimu mjumuisho wa skuli nzima kwa wote. | Kuunda kamati za elimu mjumuisho za skuli.<br>Muongozo wa kuchagua wajumbe.<br>Ufahamu wa mienendo ya madaraka<br>Ufafanuzi wa Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli<br>Sifa za mratibu wa elimu mjumuisho wa skuli.<br>Mbinu za skuli nzima |

| Moduli | Maelezo mafupi | Mada kuu zilizomo |
|---|---|---|
| | | Kuanzisha na kurekebisha misingi ya kujifunza kwa usaidizi bora wa ujumuishaji |
| **Moduli ya 3:**<br><br>**Kuwabaini Wanafunzi Walio Nje ya Skuli na Kusaidia vipindi vya Mpito katika Elimu** | Hutoa muhtasari wa suala la wanafunzi walio nje ya skuli katika mtazamo wa kitaifa na kimataifa; na kuchunguza kwa nini baadhi ya wanafunzi wako nje ya skuli, na mlolongo wa sababu na athari zinazopelekea kutokuwepo skuli.<br><br>Moduli pia inatoa mawazo ya kukuza ufaulu wa wanafunzi walio katika kipindi cha mpito. Mpito katika elimu unaelezea wanafunzi wanaoondoka, wanaokuja au wanafunzi wapya waliowasili katika mazingira mapya ya elimu, au wanaohama katikati ya mwaka. Mpito unaweza kuwa kutoka nyumbani Kwenda kituo cha elimu ya maandalizi, kutoka maandalizi Kwenda skuli ya msingi na kisha elimu ya sekondari na elimu ya juu, kutoka elimu hadi kuajiriwa, na kadhalika. | Mbinu zinazozingatia haki kwa wanafunzi walio nje ya skuli<br><br>Mifumo ya sera na sheria<br><br>Watoto walio nje ya skuli Zanzibar<br><br>Mikakati na suluhisho<br><br>Kufahamu mpito kwa ngazi za elimu<br><br>Kusimamia mpitp jumuishi<br><br>kupanga ushauri wa<br><br>Orodha hakiki za walimu<br><br>Uchunguzi<br><br>Tathmini binafasi ya skuli |
| **Moduli ya 4:**<br><br>**Uchunguzi na Utambuzi wa Mahitaji ya Kujifunza** | Husaidia kuondoka kutoka katika 'mahitaji maalum' / mkabala wa matibabu ili kutambua mahitaji ya kujifunza ya wanafunzi, na kuhimiza mbinu ambayo inalenga kutambua vikwazo vinavyoathiri kujifunza na makuzi (mbinu ya mkabala wa 'kijamii'). | Mbinu jumuishi za elimu kwa vitendo<br><br>Misingi jumuishi ya utambuzi, uchunguzi na upimaji |

| Moduli | Maelezo mafupi | Mada kuu zilizomo |
|---|---|---|
| | | Mitindo ya kujifunza<br>Vikwazo katika elimu<br>Athari za ulemavu katika kujifunza<br>Kufahamu mazingira yanayomuathiri mwanafunzi<br>Kuandaa usaidizi kwa mwanafunzi na kwa skuli |
| **Moduli ya 5:**<br>**Kuandaa Mipango binafsi ya kielimu na vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia** | Inasaidia uelewa wa mpango binafsi wa elimu (IEP) ni nini, sifa zake, na sababu kwa nini skuli ziandae na kutumia IEP; na inaangalia baadhi ya manufaa ya IEP na wanafunzi wepi wanaweza kufaidika wakiandaliwa IEP.<br>Hutoa ushauri kwa wakufunzi wa wakufunzi kutengeneza vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa kutumia nyenzo zinazopatikana ndani ya nchi. | Ufafanuzi wa Mipango binafsi ya Elimu<br>Ni nini kinajumuisha IEP<br>Namna ya kuandaa IEP<br>Kushirikiana katika kuandaa IEP<br>Kuendesha mikutano ya IEP yenye mafanikio<br>Kufuatilia, kupitia na kurekebisha IEP<br>Kutambua vifaa vya kufundishia na kujifunzia<br>Kutengeneza vifaa vya kufundishia na kujifunzia |

| Moduli | Maelezo mafupi | Mada kuu zilizomo |
|---|---|---|
| **Moduli ya 6:**<br>**Kukuza ujifunzaji Mahiri Darasani** | Hutoa mawazo kwa ajili ya mikakati jumuishi ya ufundishaji kwa ajili ya ujifunzaji mzuri ambayo yanafaa katika mazingira tofauti, ikijumuisha skuli zenye uhaba wa nyenzo na madarasa yaenye wanafunzi wengi sana. Mikakati hii inasaidia utofautishaji wakati wa ufundishaji na kuangalia ufanisi wa vikundi vya wanafunzi wenye uwezo tofauti katika kukuza mafanikio. | Ujifunzaji mahiri<br>Kazi za vikundi<br>utofautishaji katika ufundishaji na ujifunzaji<br>Kuandaa madarasa - mazingira ya darasa na kisaikolojia<br>Kuuliza masuali<br>Mrejesho<br>Kutathmini ujifunzaji |
| **Moduli ya 7:**<br>**Kukuza Ushiriki wa Mwanafunzi** | Huwawezesha walimu kukuza zaidi ushiriki wa wanafunzi katika skuli yao kupitia usaidizi wa rika, ushauri wa rika, ufundishaji rika, na kuwashirikisha wanafunzi katika kufanya maamuzi yanayowahusu. | ushiriki wa wanafunzi<br>Kukuza usaidizi wa rika<br>Kukuza ujifunzaji wa kujitegemea na fikra nzuri<br>Mazingira yanayosaidia na maeneo salama<br>Vikwazo vya ushiriki |
| **Moduli ya Ziada:** | Hutoa taarifa za msingi kuhusu mahitaji mbalimbali ya ziada, jinsi ya kutambua mahitaji ya ziada, jinsi mahitaji ya ziada yanavyoweza kuwatenga wanafunzi na | Utambuzi wa ulemavu |

| Moduli | Maelezo mafupi | Mada kuu zilizomo |
|---|---|---|
| **Ikiwa ni pamoja na Wanafunzi wenye Mahitaji ya Ziada** | vidokezo vya vitendo na mawazo kwa walimu juu ya kuwasaidia wanafunzi wenye mahitaji ya ziada katika mazingira ya skuli na darasani. | Kuelewa vikwazo vinavyowakabili wanafunzi wenye ulemavu maalum.<br><br>Mbinu za vitendo na vidokezo kwa walimu kuhusu<br>• Ulemavu wa kufahamu au kujifunza<br>• Changamoto za matamshi na mawasiliano<br>• Matatizo ya kitabia, kihisia na kijamii<br>• Ulemavu wa uoni<br>• Ulemavu wa usikivu<br>• Ulemavu wa Viungo<br>• Matatizo ya kiafya<br>• Ulemavu zaidi ya mmoja<br>• Wanafunzi wenye vipawa na vipaji. |

## B. Warsha za Mafunzo ya Wakufunzi (ToT)

Mwongozo wa mafunzo hutolewa kupitia warsha za wakufunzi (ToT), ambapo moduli moja hutolewa kwa kila warsha. Katika warsha hizi wakufunzi wa walimu:

- hujifunza kuhusu mada zinazohusiana na ujumuishaji watakazofundisha walimu;
- wanapata uzoefu wa ufundishaji/mbinu inayomlenga mwanafunzi ambayo ni muhimu kwa wakufunzi na walimu wenye ufanisi na jumuishi;
- hujifunza kuhusu, na kuchangia na kuimarisha moduli za mafunzo na kuzifanya ziwe katika mazingira ya ndani.

Msururu wa warsha hufanyika kwa angalau miaka miwili. Hii inahakikisha kuwa wakufunzi hawaelemewi na taarifa nyingi mpya kwa wakati mmoja. Watakuwa na wakati mzuri wa kuyafanyia kazi vizuri yaliyomo kwenye mafunzo na mbinu zake. Kiwango hiki cha muda mrefu pia kinamaanisha kwamba wana muda wa kutosha wa kusambaza mafunzo kwa kila moduli kwa walimu/skuli zao, kabla ya kurejea kama kikundi ili kujifunza na kuandaa moduli inayofuata.

# C. Mbinu

Mafunzo yaliyoainishwa katika mwongozo yanalenga katika kutumia mbinu shirikishi za kujifunza. Inafuata kanuni hii ya msingi:

> **Ni lazima tutumie mbinu jumuishi za mafunzo ikiwa tunataka kuwafunza wengine kwa mafanikio jinsi ya kufundisha kwa kuzingatia ujumuishi.**

Ukuzaji wa walimu huwa na ufanisi zaidi wakati shughuli za mafunzo zinaakisi mazoezi mjumuisho yanayotarajiwa kutoka kwa walimu darasani. Wakati wa vipindi vya mafunzo vilivyotolewa katika mwongozo huu, kwa hivyo, washiriki daima wanapewa uzoefu wa moja kwa moja wa kujifunza kwa maingiliano, kupitia kazi ya kikundi, kazi ya jozi, urafiki, na shughuli zingine zinazojibu mitindo tofauti ya kujifunza.

Upangaji mzuri wa chumba ni kuwa na washiriki wanaofanya kazi katika vikundi vidogo karibu na meza, kwa mfano washiriki 4-6 kwa kila jedwali. Jedwali linapaswa kuwa kubwa vya kutosha kutoshea karatasi ya chati mgeuzo na kwa vikundi kufanya kazi kwa raha, kuvaa barakoa na umbali wa kijamii ambapo kanuni za usalama za Covid-19 zinatumika. Jedwali zinapaswa kuwekwa ili kila mtu aweze kusogeza viti vyao kwa urahisi ili kuona sehemu ya mbele ya chumba au ukuta ambapo PowerPoints zinaonyeshwa, wakati wowote inapobidi. Lazima kuwe na nafasi ya kutosha kati ya meza ili kuhakikisha ufikiaji na urahisi wa harakati kwa mkufunzi na wafunzwa.



Mfano wa chumba cha warsha kilichowekwa kwa kazi ya kikundi

**[Maelezo ya picha: Chumba kikubwa chenye meza za mraba, zilizotandazwa ili kila meza iwe na viti 5-6 kukizunguka. Viti vingi vinakaliwa na washiriki wa kiume na wa kike. Nafasi pana kati ya meza hufanya chumba kiwe na nafasi kubwa.]**

Kujiendeleza kitaalamu huleta tofauti zaidi kwa walimu ikiwa:

- ni thabiti na kunazingatia mazingira ya darasani;
- kunaleta utaalamu kutoka nje ya skuli;
- kunahusisha walimu katika kuchagua maeneo ya kuendeleza na shughuli za kufanya;
- kuwezesha walimu kufanya kazi kwa ushirikiano na wenzao;
- hutoa fursa za ushauri na mafunzo;
- inaendelezwa kwa muda mrefu;
- inaungwa mkono na uongozi bora wa skuli[1].

Ndani ya kila sehemu kuna shughuli zilizoandikwa kama shughuli 'Kuu' na nyengine zimeandikwa kama shughuli za 'Ziada'.

**KUU**

Shughuli 'Kuu'za mafunzo zimeandaliwa ili kuwasaidia wakufunzi kushughulikia kwa ukamilifu mitindo mbalimbali ya kujifunza ya washiriki wao. **Shughuli hizi zinapaswa kutumika kwa urahisi, kwa kukabiliana na mahitaji ya washiriki, maslahi, na kiwango kilichopo cha ujuzi na uzoefu.** Mpangilio na muda wa shughuli zinazotolewa hapa ni mwongozo tu, si maagizo ambayo hayapaswi kubadilishwa. Baadhi ya shughuli zitahitaji muda zaidi au pungufu kuliko ilivyopendekezwa, kulingana na ukubwa wa kikundi, viwango vyao vya uelewa na/au nia ya kuchunguza masuala fulani kwa undani zaidi, kama unatumia ukalimani wa lugha/lugha ya alama, na kadhalika.

**Ziada**

Shughuli za ‘Ziada’ zinaweza kutolewa ikiwa kuna muda wa kutosha na/au ikiwa mkufunzi anahisi kuwa washiriki wake watafaidika kwa kuzifanya.

Wanahitaji kuangalia jinsi walivyowezesha shughuli au kueleza mada fulani, na kufikiria kwa kina kuhusu mafanikio yake na jinsi wanavyoweza kuiboresha katika warsha ya baadaye. Shughuli za tathmini ya warsha zinapaswa kutumika kuibua maoni ya washiriki kuhusu maudhui na mbinu ya mafunzo. Wakufunzi wanaweza kutumia madaftari yao ya kuwekea kumbukumbu za tafakuri na kutafakari kazi zao za mafunzo/uwezeshaji.

---

[1] From Walter, C. and Briggs, J. (2012). ‘What professional development makes the most difference to teachers? Oxford University Department of Education.

# D. Ujuzi wa mawasiliano

Iwe tunafunza kwenye warsha, au tunafundisha darasani, ni muhimu kuhakikisha kwamba tunawasiliana kwa ufanisi na kwa urahisi iwezekanavyo na kila mtu. Hapa kuna miongozo muhimu ya mawasiliano kwa wakufunzi kufuata na kuwahimiza washiriki kufuata:

- Zungumza na/au tumia lugha ya alama kwa uwazi na kwa kasi ambacho kila mtu anaweza kuelewa.
- Tunaweza kutamka au kusaini maneno tofauti kulingana na tunakotoka, kwa hivyo fahamu hili.
- Unapowasiliana katika kikundi na mtu ambaye ana ulemavu wa uoni, jijulishe kwa kusema jina lako ili kujitambulisha.
- Unapowasiliana katika kikundi na mtu ambaye ana ulemavu wa usikivu, jijulishe kwa kuinua mkono wako. Hakikisha unamkabili ili aweze kuona midomo yako ikitembea.
- Jitambulishe tena kwa watu iwapo wamesahau jina lako.
- Uliza ufafanuzi ikiwa huelewi kitu.
- Unapofanya kazi katika vikundi vidogo, waulize wenzako wakueleze kama huelewi kitu.
- Jaribu kutumia mbinu tofauti za mawasiliano, k.m., ishara, michoro, n.k.
- Unapoandika kwenye chati mgeuzo, tumia herufi kubwa, zinazosomeka vizuri katika rangi iliyokolea kama vile bluu au nyeusi.
- Wakati wa kufanya kazi katika vikundi, baadhi ya watu hukaa kimya huku wengine wakiwa ni wazungumzaji sana. Hakikisha kila kikundi kina mwezeshaji, mwandishi na mtu ambaye atatoa taarifa kwa kikundi kikuu.

# E. Nini Elimu Mjumuisho?

Elimu mjumuisho ni mchakato wa kuongeza uwepo, ushiriki na ufaulu wa wanafunzi wote katika mazingira ya elimu: maandalizi, skuli za msingi, skuli za sekondari na vyuo vya elimu ya juu.

Elimu kwa wanafunzi wote ina maana kwa watoto wote wa kike na kiume, na watu wazima vijana bila ya kujali jinsia zao, wanaotoka katika makabila makubwa na madogo, wakimbizi, wanafunzi wanaoomba hifadhi, wanafunzi wasio na makazi, wanafunzi wenye mahitaji ya ziada na wasio na mahitaji ya ziada, wanafunzi wenye matatizo ya kiafya, , na watoto wa mitaani, wanaofanya kazi pamoja na watoto yatima, miongoni mwa wengine. Inahusisha kurekebisha tamaduni, sera na desturi katika skuli ili ziweze kukabiliana na utofauti wa wanafunzi wote katika jamii zao.

Elimu mjumuisho inajengwa juu ya ufahamu kwamba kutengwa katika elimu hutokea kwa sababu ya matatizo ya kimsingi katika mfumo wa elimu au skuli – haielekezi 'lawama' ya ‘kutengwa’ kutokana na tabia au uwezo binafasi wa mwanafunzi. Kwa hivyo, kupitia mbinu ya elimu mjumuisho tunataka kuleta mabadiliko katika skuli, mfumo wa elimu na jamii ya karibu - mfumo - ili skuli na mazingira mengine ya kielimu iweze kumkaribisha na kumuelimisha kikamilifu mwanafunzi yeyote, ikiwa ni pamoja na wale walio na mahitaji ya ziada. Elimu mjumuisho hailengi hasa katika kubadilisha vipengele vya mwanafunzi (kimwili au kiakili). Hii haituzuii kufanya shughuli nyengine ambazo zinaweza kuwa za manufaa kwa ustawi wa kimwili na kiakili wa mwanafunzi. Haifanyi shughuli hizi kama ndio suluhisho la msingi au la pekee tunalojitahidi kulifanya.

Elimu mjumuisho inakubali kwamba watoto **wote**, vijana na watu wazima wanaweza kujifunza, na kwamba wanajifunza kwa kasi tofauti. Inahimiza ufundishaji unaonyumbulika, ambao unasaidia ujifunzaji tofauti, kwa kutumia njia tofauti kuendana na mitindo mbalimbali ya kujifunza.. Inatumia njia mbalimbali za kuwasaidia wanafunzi wenye mahitaji ya ziada au wanafunzi wengine waliotengwa, kulingana na muktadha wa mahali, kwa mfano, usaidizi rika, ushiriki wa wazazi/mlezi, watu wazima wanaojitolea wenye mahitaji ya ziada, mafunzo zaidi ya kazini kwa walimu wa kawaida, na kadhalika. Zaidi ya yote, elimu jumuisho ni mchakato wa matarajio/matumaini; ni jambo ambalo daima tunaendelea kulifanyia kazi, kwa sababu tunaweza kuendelea kuimarisha kila wakati. Si suluhusho la haraka - maendeleo ya elimu mjumuisho huchukua muda na inahitaji kila mtu anayehusika kujitolea kwa vitendo vya kudumu, vinavyoendelea.

# F. Mfumo wa Kujitathmini kwa walimu na skuli katika mafunzo ya elimu mjumuisho(IETT)

Kujitathmini kwa mwalimu na skuli ni mchakato muhimu ambao ni kweli hasa wakati wa kuendeleza elimu mjumuisho kwani inahusisha mabadiliko ya mfumo; daima tunahitaji kutafuta njia za kuimarisha utoaji wetu wa elimu na matendo.

Kwa kuanza na Moduli ya 3, wakufunzi wakuu wanatambulishwa mfumo wa mafunzo ya ualimu wa elimu mjumuisho (IETT)wa kujitathmini. Huu ni mfumo wa umahiri ulioundwa ili kuchangia uimarishaji wa mwalimu binafsi, idara, kamati na skuli nzima katika umahiri unaokuzwa katika moduli za mafunzo ya elimu mjumuisho kwa walimu. Umahiri umeainishwa katika 'maeneo' manne: Kufundisha na kujifunza; Maendeleo binafsi na ustawi wa wanafunzi; Kushirikisha wazazi/walezi na jamii; na Uongozi na usimamizi. Kila eneo linaandaliwa viwango vya umahiri ambavyo mwalimu huviangalia wakati wa ushiriki wao katika moduli za mafunzo ya ualimu wa elimu mjumuisho[2].

Wakufunzi wakuu (PTs) wataitambulisha zana hii ya kujitathmini kwa walimu wa skuli za majaribio na wafanyakazi wengine muhimu ili kuwawezesha kufuatilia mafanikio yao wenyewe na ujuzi wa elimu mjumuisho wanapoendelea kupitia moduli na kutumia mafunzo yao. Zana ya kujitathmini imeandaliwa ili kuwasaidia kufafanua mawazo na malengo yao ya kujifunza, na kutambua umahiri watakaoupata, na kile ambacho bado wanahitaji kujifunza. Watahimizwa kurejelea zana mara kwa mara kwao binafsi na wenzao wa skuli, na watapata fursa za majadiliano na kutafakari maendeleo yao ya mafunzo kazini kwa kila skuli ya majaribio (INSET), kama vile Wakufunzi Wakuu (PTs) kwenye warsha za Mafunzo ya Wakufunzi (ToT).

[2] The levels of competency are described as: 'beginning', 'developing', 'proficient' and 'advanced'.

# G. The Muktadha wa Kizanzibari

Katika Zanzibar, mfumo rasmi wa elimu kabla ya Mapinduzi ya 1964 haukutoa fursa kwa wanafunzi wote Kwenda skuli. Baada ya mapinduzi, elimu ilitangazwa kuwa bure kwa Wazanzibari wote bila kujali rangi, kabila, imani au jinsia. Ingawa tamko hili lilijumuisha wanafunzi wenye matatizo makubwa ya kujifunza na au ulemavu, mazingira ya kujifunzia hayakuwawezesha wanafunzi hawa kwenda skuli. Wala serikali haikuanzisha skuli maalum kwa ajili ya wanafunzi hao. Ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wote, wakiwemo wenye ulemavu wanakwenda skuli, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilianzisha Kitengo cha Elimu Maalum ndani ya Wizara mwaka 1988. Miaka mitatu baadae, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilianzisha vitengo maalum katika baadhi ya skuli, kama vile, Skuli ya Msingi Kisiwandui, Skuli ya Msingi Michakaini, Skuli ya Msingi Jang'ombe, na Skuli ya Msingi Mwembe Makumbi. Vitengo viliandikisha wanafunzi wenye ulemavu wa akili, ulemavu wa usikivu na ulemavu wa Uoni. Baadhi ya wanafunzi wana ulemavu zaidi ya mmoja. Mbali na idadi ndogo ya wanafunzi wenye ulemavu walioandikishwa katika vitengo hivyo, wapo wengine wengi ambao hawakuhudhuria skuli kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo mitazamo hasi kuhusu ulemavu na umaskini.

Ili Kwenda sambamba na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) Tamko la Salamanca (1994), Zanzibar ilianza taratibu kubadilisha mfumo wake wa elimu kuelekea ujumuishaji. Kuanzishwa rasmi kwa elimu mjumuisho katika skuli za Zanzibar kuliwezekana kwa juhudi za pamoja kati ya serikali ya Zanzibar na mashirika ya kitaifa na kimataifa yasiyokuwa ya kiserikali (NGO). Baada ya upembuzi yakinifu/utafiti wa mwaka 2004, skuli 20 za majaribio (12 kutoka Unguja na 8 kutoka Pemba) zilichaguliwa kupitia msaada wa NFU na (ODW). Hii ilifuatiwa na kuanzishwa kwa Mradi wa Elimu Mjumuisho na Maendeleo ya Vijana ambao uliendeshwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (MoEVT) na Jumuiya kwa Ajili ya Watu Wenye Ulemavu wa Akili Zanzibar (ZAPDD), kwa msaada wa fedha kutoka NFU.

Mwaka 2005, Kitengo cha Elimu Maalum kilibadilishwa jina na kuitwa Kitengo cha Elimu Mjumuisho. Tangu wakati huo, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na ZAPDD, kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo wa kimataifa (hasa NFU), zimekuwa zikifanya kazi kubwa ya kuanzisha elimu mjumuisho katika skuli za Zanzibar na kwa wadau mbalimbali wakiwemo watunga sera, viongozi wa mitaa, jumuiya za Watu wenye ulemavu (DPO) na wazazi/ walezi. Washirika wengine wa maendeleo wa kimataifa ambao pia wamesaidia kifedha maendeleo ya elimu mjumuisho Zanzibar ni pamoja na Shirika la Msaada la

Marekani (USAID), World Home for Youth (WHY), Shirika la Maendeleo la Norway (NORAD), NAD na Sight Savers International (SSI).

Hatua kubwa za kuingizwa katika mfumo wa elimu Zanzibar tangu mwaka 2006 ni pamoja na: kuingiza elimu mjumuisho katika Sera ya Elimu ya Zanzibar (2006); kuongeza idadi ya skuli 'jumuishi' kutoka skuli 20 za majaribio mwaka 2004 hadi 152 kati ya jumla ya skuli zaidi ya 1,000 ilipofika mwaka 2019; kuanzishwa kwa kozi ya elimu mjumuisho ya mwaka mmoja katika Chuo cha Kiislamu mwaka 2006; kuweka Washauri wa Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha na Wataalamu wao; kuanzishwa kwa programu ya miaka miwili ya elimu mjumuisho na mahitaji maalum katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) mwaka 2014, na kuanza kwa mchakato wa kuandaa Sera ya Elimu Mjumuisho mwaka 2010.

Kwa kuwa walimu ndio kiini cha mchakato jumuishi, mikakati kadhaa imefanywa ili kukuza uwezo wa walimu wa kutoa na kukuza ujumuishaji katika madarasa na skuli zao. Mikakati hii ni pamoja na warsha za kuwajengea uwezo walimu waliopo kazini na wale walioko vyuoni. Tokea mwaka 2005, warsha kadhaa za mafunzo ya elimu mjumuisho zimeandaliwa Unguja na Pemba.

# H. Walengwa wa mafunzo haya

## Wakufunzi wakuu

Washiriki wa awali wa mafunzo ni Wakufunzi wakuu ambao wana jukumu la kutoa mafunzo ya ualimu.

Wakufunzi Wakuu ni wadau ambao:

- Wana upendo na masuala ya elimu mjumuisho, uzoefu na ujuzi; na
- Wana jukumu la kuwafunza walimu, k.m., Mafunzo kazini, katika jukumu lao kuu la kitaalamu au ni walimu wakuu wa skuli za majaribio; na/au
- wana wajibu wa kuwafunza walimu wanafunzi katika Taasisi za ualimu katika jukumu lao kuu la kitaalamu.

Wakufunzi wakuu wana nafasi ya kuingiza majukumu ya mafunzo ya elimu mjumuisho katika maelezo yao ya sasa ya kazi na mipango kazi. Kwa mfano, wanaweza kuwa:

- Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha (IELS), Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, wafanyakazi, washauri wa kituo cha walimu (TC) na walimu wataalamu, wakufunzi wa Makuzi ya Awali (ECD);
- Taasisi za Mafunzo ya Ualimu (TTIs), k.m., wakufunzi wa vyuo na wahadhiri wa vyuo vikuu
- walimu wakuu.

Washiriki watakuwa na uzoefu mbalimbali wa kiutendaji katika elimu kuhusiana na ufundishaji, mafunzo na kufanya kazi na wanafunzi mbalimbali.

Wengine watajiamini kuhusu kuwafundisha walimu kuwa waelimishaji jumuishi. Wengine wataelewa nadharia hiyo lakini, kwa uhalisia, bado wanahisi kuwa na wasiwasi au kukataa kufanya kazi  kwa kujumuisha wengine au kuwafundisha wengine kuwajumuisha na kuwajumuisha wanafunzi wote, hasa wale wenye mahitaji ya ziada, wakiwemo wenye mahitaji maalum ya kielimu na/au ulemavu. kuanza kila kipindi cha mafunzo kwa kuanza na pale walipofikia washiriki'. Inashauriwa sana kwamba wakufunzi waanze kila moduli kwa kufanya muhtasari mfupi wa maudhui na shughuli kutoka moduli zilizopita.

Baada ya kushiriki katika warsha ya mafunzo ya wakufunzi (ToT) na kujifunza kuhusu Moduli, Wakufunzi Wakuu (PTs) huanza kutumia moduli hiyo kuwafundisha walimu katika skuli. Katika mchakato huu wao:

- hufanya kazi pamoja na wakufunzi wakuu (PTs) kwa jozi au kwa vikundi ili kuandaa na kuwezesha Mafunzo kazini kwa skuli yao ya majaribio. Skuli za majaribio kwa kawaida huchaguliwa kwa vigezo na kwa ushirikiano wa karibu na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na wadau wengine wakuu;
- Huwa na ushirikiano na wenye kutafakari wakati wa kutatua matatizo;
- kupitia kwa kina na kurekebisha jumbe za mafunzo na mbinu ili ziendane vyema na mazingira yao, mahitaji ya walimu na mitindo yao ya mafunzo.

Moduli za mafunzo katika mwongozo huu pia zitumiwe na Wakufunzi Wakuu (PT) wanapokuwa wanatoa mafunzo kwa walimu wanafunzi wakati wa mafunzo ya chuoni.

Kwa kuongezea kwa kila moduli, Wakufunzi Wakuu (PTs) hupewa mpango wa warsha wa Mafunzo kazini wa kina, mawasilisho ya Pawapointi ambayo yanaambatana na kila moduli, na nyenzo nyengine za mafunzo ili kusaidia shughuli za mafunzo.

## Waangalizi

Vipengele vya moduli vimeandaliwa ili kutoa mafunzo kwa vikundi vya **'Waangalizi'** wanaofuatilia maendeleo ya ujumuishaji katika skuli za majaribio.

Sio tu jukumu la mwalimu kutoa elimu mjumuisho. Ili kuleta mabadiliko yanayohitajika kwa ajili ya elimu mjumuisho yenye mafanikio, wadau wakuu katika mfumo mzima wa elimu na mashirika mengine husika wanatakiwa kutekeleza jukumu la kuhimiza, kufuatilia na kusimamia elimu mjumuisho. Waangalizi kwa kawaida huwa wafanyakazi wenye uzoefu mkubwa au watu wenye dhamana katika jumuiya ambao wanasaidia mpango wa Mafunzo ya Ualimu ya elimu mjumuisho na mabingwa wa ujumuishaji.

Timu ya Waangalizi

- **Chunguza matendo ya skuli:** Kabla ya mpango wa Mafunzo ya Ualimu wa Elimu Mjumuisho (IETT) kuanza skuli, kikundi cha Waangalizi hutembelea skuli ili kuona kinachofanywa darasani na kuzunguka skuli. Kisha wanatembelea skuli kila mwaka ili kuona mabadiliko, mafanikio na changamoto.

- **Zungumza na wadau wakuu:** Waangalizi huwahoji walimu, walimu wakuu, wafanyakazi wengine wakuu, wanafunzi na wanajamii ili kuangalia namna mafunzo hayo yalivyopokelewa na kutumika. Wanakusanya mawazo ya namna ya kuimarisha au kupanua mafunzo ya ualimu.
- **Rikodi maendeleo:** Waangalizi hutayarisha ripoti fupi za maandishi na picha kuhusu uchunguzi na majadiliano yao.
- **Toa mrejesho:** Waangalizi hufanya kazi kama 'marafiki'. Wanatoa mrejesho mzuri na wenye kujenga kwa wakufunzi. Pia wanatoa mrejesho kwa wawezeshaji wakuu, jumuiya zinazoongoza zinashirikishwa katika mpango na maafisa wa elimu husika.

Waangalizi wanachukuliwa kutoka jumuiya muhimu za wadau. Hao ni pamoja na:

- Maafisa wakuu wa kitaifa na wilaya na wakaguzi wakuu wa WEMA;
- wafanyakazi waandamizi wa vyuo vikuu na vyuo vya ualimu, k.m., wakuu wa vyuo/makamu wakuu/wakuu wa vitivo;
- wawakilishi wakuu kutoka Jumuiya za Watu wenye Ulemavu (DPOs) na jumuiya nyengine za kiraia;
- wawakilishi kutoka Wizara nyengine za serikali na wadau wanaohusika na watoto na vijana, kama vile wafanyakazi wa kijamii na wahudumu wa afya.

Mafunzo ya waangalizi yanajumuisha kukuza uelewa wa elimu mjumuisho, mbinu za utafiti ambazo Wakufunzi Wakuu (PT) na walimu watakuwa wakitumia, jinsi ya kutumia kifurushi cha nyenzo zinazoongoza ufuatiliaji wao wa utoaji wa elimu mjumuisho skuli, na ufahamu kuhusu maudhui ya moduli za mafunzo. Waangalizi pia wanaoneshwa jinsi ya kusaidia kuimarisha mafunzo ya walimu yanayojenga mtazamo mzuri. Jukumu lao ni kusaidia na kuhamasisha tafakuri za wakufunzi na walimu wenyewe na mapendekezo ya uimarishaji. Waangalizi wanafunzwa hasa sio wawe wakaguzi wanaotoa alama/maksi na kutathmini walimu, lakini kama 'marafiki'.